



TAARIFA KWA UMMA

TARATIBU MPYA ZA UINGIZAJI WA BIDHAA ZA CHAKULA (MALI MBICHI) VISIWANI KOMORO

Dar es Salaam- 13 Septemba, 2019

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), inapenda kuwataarifa wazalishaji na wafanyabiashara wa bidhaa za chakula kibichi, mifugo, mbogamboga na matunda yanayoingia kwenye soko la Visiwa vya Komoro kuwa, taratibu mpya za uingizaji wa bidhaa za chakula (Malimbichi) ni kama ifuatavyo;

1. Ulipaji wa ushuru kwa wanyama hai utategemea uwasilishaji wa nakala ya makubaliano pamoja na kibali cha uingizaji wa bidhaa kutoka nje ambacho hutolewa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Kilimo, Uvuvi na Mazingira (INRAPE), pamoja na cheti cha afya kilichowekwa saini na daktari wa mifugo anayekubalika na nchi husika
2. Bidhaa kama vile mbogamboga na matunda haziwezi kuruhusiwa kuingia nchini humo bila kuwa na *Phytosanitary Certificate* kilichotolewa na nchi husika bidhaa inapotoka, cheti cha afya (*Health Certificate of Conformity*) pamoja na kibali kilichotolewa na Mamlaka ya Afya (*Phytosanitary*) cha INRAPE
3. Kwa upande wa pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu, kutategemea uwasilishaji wa makubaliano na kibali cha uingizaji wa bidhaa hizo kutoka nje, kilichotolewa na INRAPE

Hivyo, tunaomba wazalishaji na wafanyabiashara wa bidhaa tajwa kuzingatia taratibu za uingizaji ili kuepuka usumbufu na uharibifu wa bidhaa zao endapo watahindwa kuzingatia taratibu hizo.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu namba 0735647165 (Bi. Lulu Adam)

Imetolewa na;

Theresa H. Chilambo
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano